

**SALAMU ZA MHE. DKT. DAMAS NDUMBARO (Mb), MWENYEKITI WA KAMATI
YA KUDUMU YA BUNGE UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KWA MHE.
RIDHIWANI KIKWETE (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI
YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI WA KUFUNGA KIKAO
KAZI CHA SITA (6) CHA SERIKALI MTANDAO TAREHE 19 FEBRUARI, 2026
KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb); Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ,

Mhe. Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Ndg. Mululi Mahendeka; Katibu Mkuu Ikulu

Makatibu Wakuu wote,

Dkt. Mussa Kisaka; *Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,

Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali

Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo/Sehemu, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;

Viongozi wa Dini,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana,

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa na kukamilisha kwa mafanikio **kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao**. Kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, napenda kutoa

pongezi za dhati kwa uongozi na watendaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa maandalizi mazuri ya kikao hiki pamoja na kazi kubwa mnayoendelea kuifanya katika kuratibu na kusimamia ajenda ya Serikali Mtandao.

Mhe. Waziri,

Kikao kazi hiki kimekuwa jukwaa muhimu la kutathmini utekelezaji wa miradi ya TEHAMA Serikalini, kubaini mafanikio yaliyopatikana, kujadili changamoto zilizopo, pamoja na kuweka mikakati ya kuimarisha utoaji wa huduma za umma kwa njia za kidijitali. Kamati imefarijika kuona hatua zinazochukuliwa katika kuunganisha mifumo ya Serikali, kuimarisha usalama wa taarifa, na kuongeza upatikanaji wa huduma za kielektroniki kwa wananchi.

Kwa dhati kabisa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria **inaipongeza e-GA kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake** kwa mujibu wa sheria na miongozo ya Serikali Mtandao. Kamati **imeridhishwa** na namna e-GA inavyoratibu matumizi ya TEHAMA Serikalini, kudhibiti urudufu wa mifumo, kusimamia viwango na usalama wa mifumo ya kidijitali, pamoja na kuhakikisha miradi ya TEHAMA inaleta thamani halisi za fedha za umma.

Aidha, Kamati imeridhishwa na juhudi za e-GA katika kusimamia na kuzishauri Wizara, Idara na Taasisi za Umma katika utekelezaji wa miradi ya TEHAMA, jambo ambalo limechangia kuongeza uwazi, uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Bunge la Tanzania ni miongoni mwa wanufaika wa huduma za Serikali Mtandao, kwani sasa Bunge letu kwa sehemu kubwa, halitumii makaratasi tena bali mfumo wa kidigitali wa kuendesha shughuli za Bunge **wa e-Parliament** uliojengwa na e-GA kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge. Haya ni mafanikio yanayostahili pongezi na kuungwa mkono zaidi.

Mhe. Waziri,

Napenda kulihakikishia Bunge na Serikali kwa ujumla kuwa, Kamati itaendelea kutekeleza kikamilifu jukumu lake la kikatiba la **kuisimamia, kuishauri na kuifuatilia e-GA**, ili kuhakikisha jitihada za Serikali Mtandao zinaimarika na kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia duniani. Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji wa sheria na miongozo ya Serikali Mtandao, sambamba na kuhakikisha uwajibikaji na matumizi bora ya rasilimali za umma katika miradi ya TEHAMA Serikalini.

Vilevile, Kamati itaendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara yako ambayo imepewa dhamana ya kusimamia Serikali Mtandao, Wizara ya Fedha pamoja na Wizara, Idara na Taasisi zote za Umma, ili kuhakikisha ajenda ya Serikali Mtandao inatekelezwa kwa ufanisi, mifumo inaunganishwa ipasavyo, na huduma za kidijitali zinamfikia mwananchi kwa urahisi na kwa wakati.

Mhe. Waziri,

Kamati inatambua kuwa, mafanikio ya Serikali Mtandao yanahitaji **rasilimali za kutosha**, hususan upande wa bajeti. Katika muktadha huo, Kamati itaendelea kuishauri Serikali na Bunge kuona umuhimu wa **kuongeza na kuimarisha bajeti ya e-GA**, ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, ikiwemo kuendeleza miundombinu ya TEHAMA, kuimarisha usalama wa mifumo, kujenga uwezo wa watumishi wa umma, na kuhakikisha mifumo yote ya Serikali inafanya kazi kwa ufanisi na kwa viwango vinavyokubalika.

Kamati inaamini kuwa, uwekezaji katika Serikali Mtandao si gharama bali ni uwekezaji wa kimkakati unaochochea maendeleo, unaoongeza mapato ya Serikali, unapunguza gharama za uendeshaji, na kuboresha maisha ya wananchi.

Mhe. Waziri,

Mwisho, napenda kuwashukuru washiriki wote wa kikao kazi cha 6 cha Serikali Mtandao kwa michango yenu ya kina na ushiriki wenu wa dhati. Kamati ina matarajio makubwa kuwa maazimio na mapendekezo yaliyotolewa yatafanyiwa kazi kikamilifu kwa manufaa ya Taifa letu.

Ahsanteni kwa kunisikiliza,

Kazi na Utu....